# WIZARA YA AFYA

## BARAZA LA FAMASI

# TAARIFA KWA UMMA

Ofisi ya Msajili wa Baraza la Famasi imepokea kwa masikitiko taarifa iliyotolewa kupitia Gazeti la JAMHURI la tarehe 15 – 21 Novemba 2022, Ukurasa wa 5, yenye kichwa cha habari **"Mfamasia 'amnywesha' mgonjwa dawa ya upele".**

Katika ufuatiliaji wa awali, imebainika kuwa mhusika aliyetoa dawa hizo ni **MWANAFUNZI** wa ngazi ya cheti (Astashahada – NTA L5) kutoka Chuo cha *Hermargs Institute* ambaye alikuwa kwenye mafunzo kwa vitendo *(field)* katika Hospitali ya Turiani St. Francis, Mvomero.

Kiutaratibu mwanafunzi anapokuwa kwenye mafunzo anapaswa kuwa chini ya usimamizi na uangalizi wa mwanataaluma ambaye amesajiliwa na kutambuliwa na Baraza la Famasi.

Kutokana na kuwepo kwa taarifa hizi, Ofisi ya Msajili inawaomba wananchi kuendelea kuwa watulivu wakati suala hili linaendelea kufanyiwa kazi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wote watakaobainika kuzembea katika kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za kitaaluma.

Natoa wito kwa wasimamizi wa mafunzo ya vitendo (*field*) katika taaluma ya famasi ngazi zote ,kuzingatia taratibu za usimamizi wa wanafunzi wanapokuwa katika mafunzo ili kuepukana na madhara yanayoweza kusababishwa na utoaji wa dawa usio sahihi na kusababisha athari kwa wagonjwa.

**Elizabeth Shekalaghe**
**MSAJILI, BARAZA LA FAMASI**
**17 Novemba, 2022**